

## **Maswali Kuhusu Fidia kwa Wafanyakazi na Virusi vya Korona (COVID-19)**

**1. Je, malipo yangu ya upotevu muda yataendelea?**

Ndiyo. Ikiwa huwezi kufanya kazi kutokana na majeraha au ugonjwa unaohusiana na kazi, malipo yako ya upotevu wa muda yataendelea.

**2. Je, nawezaje kupata taarifa kuhusu hali ya madai yangu?**

Pata taarifa zinazotumwa kiotomatiki kwa Kiingereza au Kihispania kwa kupiga simu **1-800-831-5227**

**3. Je, amri na tangazo vitakuwa vya mwisho ikiwa siwezi kupata barua wakati shughuli yangu imefungwa?**

Ikiwa huwezi kupata amri kwa kosa lisilo lako, naweza kumweleza msimamizi wa malalamiko kama vile hukuweza kupata barua yako.

**4. Je, kupokea malipo ya kujikimu ya serikali kuu kunaathiri kiasi cha malipo yangu ya upotevu wa muda au mafao ya uzeeni?**

Hapana.

**5. Je, ninaweza kupata miadi ya matibabu na mafunzo ya ufundi kwa njia ya simu?**

Ndiyo.

**6. Daktari wangu wa viungo hataweza kuniona kwa sasa. Nifanyaje?**

Muulize mtoa huduma wako kama anatoa machaguo ya huduma ya afya masafa au kama unaweza kuwasiliana nao kwa simu.

**7. Bima yang ya afya imezuiwa. Je, hili linaathilije madai yangu?**

Madai yako hayatafungwa ikiwa unahitaji matibabu zaidi. Tutakupatia muda wa kukamilisha bima yako ya afya pale huduma za afya zitakaporejea.

**8. Ningependa kuahirisha au kupanga upya uchunguzi huru wa matibabu (IME) kwa sababu nina wasiwasi juu mlipuko wa virusi vya korona. Nifanyaje?**

Wasiliana na msimamizi wako wa madai angalau siku 5 za kazi kabla ya miadi yako ili kupata ufumbuzi.

**9. Je, ni sahihi kughairisha au kusogeza mbele miadi au taratibu za matibabu kwa sababu ya wasiwasi wa virusi vya korona?**

Wasiliana na mtoa huduma ya afya ili kujua kile wanachopendekeza.

**10. Tangu shule ya mtoto wangu ifungwe, sina huduma za mtoto na nahitaji kusogeza mbele miadi ya matibabu au ya ufundi. Nifanyaje?**

Fanya kila jitihada kupanga huduma ya watoto. Kama haiwezekani, wasiliana na mnasahi wa ukarabati wa mafunzo ya ufundi (VRC) au mtoa huduma ya matibabu.

**11. Nina wasiwasi kuhusu kwenda darasani au kushiriki katika mpango wangu wa kufunzwa tena kwa sababu ya virusi Nifanyaje?**

Wasiliana na VRC wako ili kuangalia machaguo.

**12. Kazi yangu nyepesi ya muda mfupi haipatikani tena kwa sababu ya virusi. Nifanyaje?**

Wasiliana na msimamizi wangu wa madai.

**13. Mwajiri wangu amenisimamisha kazi kwa sababu ya mlipuko wa virusi vya korona na nina madai ambayo hayajafungwa. Je, hili linawezaje kuathiri mafao yangu?**

Bado tutaidhinisha matibabu stahiki ya kwenye madai yako. Tutakupa muda kukamilisha matibabu yako kabla ya kufunga madai yako.

**14. Nimetolewa kazini, lakini sina kazi ya kuirejea, na soko la ajira ni dogo sana kutokana na mlipuko wa virusi vya korona. Nifanyaje?**

Kwa bahati mbaya, idara hawezi kulipa mafao ya upotevu wa muda mara baada ya kuweza kurudi kazini. Unaweza kustahiki mafao ya ukosefu wa ajira kupitia Employment Security Department.

**15. Je, L&I inaruhusu COVID-19 kama mazingira yanayohusiana na kazi?**

Katika mazingira fulani, pale kazi ya wafanyakazi inapokuwa na uwezekano mkubwa wa kuambukizwa ugonjwa kwa sababu ya kazi (mifano ni pamoja na washughulikiaji wa kwanza au wafanyakazi wa huduma za afya). Lazima kuwe na hatari iliyo katika kumbukumbu au hatari inayohusiana na kazi, na uhusiano wa mfanyakazi/mwajiri.

**16. Je, lini L&I itakataa madai?**

Pale maambukizi ya COVID-19 yanapokuwa bahati mbaya mahali pa kazi (kama vile mfanyakazi wa ofisini ambaye ameambukizwa kutoka kwa mfanyakazi mwenzake).

**17. Je, nawezaje kuwasilisha madai ya COVID-19?**

Kwa njia ya simu: **1-877-561-3453**

Katika ofisi ya daktari wako (unapojaza Ripoti ya Ajali).